

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



MTAALA NA MUHTASARI WA ELIMU YA AWALI
2023

©Taasisi ya Elimu Tanzania 2023
Toleo la kwanza 2023

ISBN 978-9987-09-819-4

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P 35094
14112 Dar es Salaam.

Simu: +255 735 041 168 / 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Mtaala huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). *Mtaala wa Elimu ya Awali*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha wala kutafsiri andiko hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Kamishna wa Elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Yaliyomo

Orodha ya Majedwali.....	v
Vifupisho.....	vi
Shukurani.....	vii
Dibaji.....	ix
Sehemu ya Kwanza: Mtaala wa Elimu ya Awali	x
Utangulizi.....	1
1.1 Usuli.....	1
1.2 Muundo wa Elimu ya Awali.....	1
Dira, Malengo na Umahiri wa Jumla.....	1
2.1 Dira	1
2.2 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania	2
2.3 Malengo ya Elimu ya Awali	2
2.4 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Awali.....	3
Maudhui ya Mtaala	3
3.1 Utamaduni, elimu ya imani, sanaa na michezo.....	4
3.2 Lugha na mawasiliano	4
3.3 Stadi za awali za maisha	4
3.4 Afya na mazingira.....	4
3.5 Stadi za awali za kihisabati, kisayansi na TEHAMA.....	4
Ufundishaji, Ujifunzaji na Upimaji.....	6
4.1 Ufundishaji na ujifunzaji.....	6
4.2 Uchopekaji wa masuala mtambuka	6
4.3 Muda wa kujifunza	7
4.4 Lugha ya kufundishia na kujifunzia	9
4.5 Upimaji wa maendeleo ya mtoto	9
Rasilimali za Utekelezaji wa Mtaala.....	9
5.1 Rasilimali watu	9
5.2 Rasilimali vitu.....	11
5.3 Miongozo muhimu ya usimamizi na uendeshaji wa shule.	12
5.4 Rasilimali muda	12
5.5 Rasilimali fedha	12

5.6 Ushiriki wa wadau katika utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Awali	12
Sehemu ya Pili: Muhtasari wa Elimu ya Awali	13
1.0 Utangulizi.....	14
2.0 Maudhui ya ufundishaji na ujifunzaji	14
Bibliografia	30

Orodha ya Majedwali

Jedwali Na.1.1: Maeneo ya Ujifunzaji na Umahiri Mkuu	3
Jedwali Na.1.2: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi	5
Jedwali Na.1.3: Masuala Mtambuka.....	6
Jedwali Na.1.4: Utaratibu wa Ujifunzaji kwa Siku.....	8
Jedwali Na.1.5: Muda wa Ufundishaji na Ujifunzaji kwa Wiki	8
Jedwali Na.2.1: Maudhui ya Muhtasari wa Elimu ya Awali.....	15

Vifupisho

LAT

TEHAMA

TET

WyEST

Lugha ya Alama Tanzania

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Taasisi ya Elimu Tanzania

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Shukurani

Maandalizi ya mtaala huu yamehusisha wadau mbalimbali kutoka sekta za umma na binafsi. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha kupatikana kwa Mtaala na Muhtasari wa Elimu ya Awali. Hivyo, TET inatoa shukurani za dhati kwanza, kwa Kamati ya Kitaifa ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda (Mb.). Kamati hiyo ilikuwa na wajumbe kumi (10), wakiongozwa na Mwenyekiti wake Prof. Makenya Abraham Maboko. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi kuhakikisha kuwa mtaala huu unaandaliwa kwa wakati na unakidhi shauku ya wadau juu ya ubora wa elimu ya awali.

Pili, shukurani ziende kwa taasisi, wizara na wadau mbalimbali wa elimu walioshiriki kutoa maoni kuhusu uboreshaji wa mtaala. Baadhi ya taasisi, wizara na wadau hao ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Baraza la Wawakilishi Zanzibar, wajumbe wa Kamati ya Mapitio ya Sera ya Elimu, wajumbe wa Kamati ya Kufanya Mageuzi Makubwa ya Elimu Zanzibar, viongozi wa dini, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Taasisi ya Elimu Zanzibar, Bodi na Menejimenti za Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Tanzania, menejimeti na wakufunzi wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume, Chuo cha Amali Zanzibar, Baraza la Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Ufundi Stadi, Baraza la Mitihani Tanzania, Chama cha Walimu Tanzania na Baraza la Watoto na Vijana Balehe Tanzania. Vilevile, wadau wengine ni wajumbe wa bodi za shule, wanafunzi wa shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu, walimu wa shule za msingi, sekondari, wakufunzi wa vyuo vya ualimu, wahadhiri wa vyuo vikuu, waajiri, wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu, Tume ya Vyama vya Ushirika, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Akademia ya Sayansi Tanzania, Benki Kuu ya Tanzania na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Kimataifa.

Tatu, TET inayashukuru mashirika ya United Nations International Children's Fund, United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization, Room to Read, Right to Play, Data Vision, Plan International, Norwegian Refugees Council, Christian Social Services Commission, Global Education Link, UWEZO, Hill Packaging Ltd., Teacher Education Support Project, Madrasa Early Childhood Programme – Zanzibar, Morale Foundation for Education and Training na Educate! kwa kufadhili hatua mbalimbali za uandaaji wa mitaala.

Nne, TET inatoa shukurani za dhati kwa wataalamu wote wa elimu ya awali kutoka ndani na nje ya TET walioshiriki kuandaa mtaala huu. Mwisho, ingawa si kwa umuhimu, TET inaishukuru sana Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) kwa kuwezesha kazi ya uandishi, uchapaji na usambazaji wa mtaala huu.



Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania

Dibaji

Mtaala wa Elimu ya Awali umeandaliwa kwa kuzingatia *Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014* Toleo la Mwaka 2023, maoni ya wadau yaliyokusanywa na kuchakatwa mwaka 2021 hadi 2022 na matokeo ya uchambuzi wa maandiko kuhusu uzoefu kutoka nchi nyingine. Aidha, mtaala huu unazingatia dira ya elimu ambayo inalenga kumwandaa Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo katika kuleta maendeleo endelevu ya kitaifa na kimataifa. Vilevile, mtaala huu umezingatia malengo makuu ya elimu pamoja na malengo ya elimu ya awali nchini Tanzania. Kwa kuzingatia haya, mtaala huu umeweka viwango vya utoaji wa elimu katika ngazi ya Elimu ya Awali kwa kubainisha maarifa, stadi na mwelekeo atakaoujenga mtoto, umahiri wa jumla, maeneo makuu ya ujifunzaji, umahiri mkuu na mahususi pamoja na njia za ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, mtaala umebainisha muda utakaotumika katika utekelezaji, lugha ya kujifunzia na kufundishia, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na njia zitakazotumika katika upimaji wa maendeleo ya mtoto kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri. Vilevile, mtaala umebainisha sifa za kitaaluma na kitaalamu za mwalimu ambaye ndiye mtekelezaji mkuu wa mtaala katika ngazi ya shule.

Pamoja na matamko mbalimbali ya kisera na miongozo ya kitaifa, kikanda na kimataifa, mtaala huu umezingatia nadharia za ukuaji na ujifunzaji wa mtoto na Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea. Falsafa hiyo inasisitiza utoaji wa elimu inayomwezesha Mtanzania kujitegemea na kumudu maisha yake ya kila siku. Hivyo, utekelezaji wake utawezesha ukuaji wa mtoto kimwili, kiakili, kihisia na kijamii. Ni matarajio yangu kuwa kupitia mtaala huu, mwalimu atamwezesha mtoto kujenga umahiri uliokusudiwa. Wasimamizi wote wa utekelezaji wa mtaala na wadau wengine wa Elimu ya Awali nchini watahakikisha kuwa elimu inayotolewa inakidhi viwango vya ubora vinavyokubalika kitaifa, kikanda na kimataifa.



Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa

Kamishna wa Elimu

SEHEMU YA KWANZA
MTAALA WA ELIMU YA AWALI

Utangulizi

1.1 Usuli

Nchi nyingi duniani, ikiwemo Tanzania, zinatambua kwamba elimu ni haki ya kila mtoto, na hivyo zimekuwa zikifanya jitihada mbalimbali kuhakikisha kuwa elimu bora inatolewa kwa haki na usawa. Jitihada hizi zinafanyika kutokana na ukweli kwamba elimu ni nyenzo muhimu katika maendeleo ya kila mtoto na katika ukuzaji wa vipaji mbalimbali. Malengo ya elimu kwa wote yaliyotamkwa na Azimio la Dunia la Jomtien la mwaka 1990 na Itifaki ya Dakar ya mwaka 2000 yamesisitiza utoaji wa elimu bora kwa wote bila ubaguzi (UNESCO, 2020). Makubaliano ya Salamanca ya mwaka 1994 pia, yamesisitiza utoaji wa elimu jumuiishi inayozingatia mahitaji maalumu ya mtoto. Sanjari na hayo, lengo la nne la Maendeleo Endelevu la Umoja wa Mataifa la mwaka 2015 linasisitiza kila nchi kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata nafasi ya kujiunga na elimu ya awali ili kuwaandaa kwa ajili ya elimu ya msingi. Vilevile, Kiunzi cha Ustawi, Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto cha mwaka 2018, kinafafanua umuhimu wa utoaji wa elimu ya awali kwa kuwajengea watoto utayari wa kuanza elimu ya msingi na ukuaji wao katika nyanja zote. Aidha, Mtaala huu unazingatia falsafa ya Elimu ya Kujitegemea ya mwaka 1967 kama ilivyoainishwa kwenye Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 Toleo la Mwaka 2023. Halikadhalika, mwalimu anashauriwa kuchagua na kutumia nadharia za ujifunzaji na ufundishaji zinazoendana na falsafa hiyo.

1.2 Muundo wa Elimu ya Awali

Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 Toleo la Mwaka 2023 inaelekeza Elimu ya Awali itolewe kwa muda wa mwaka mmoja. Mtoto ataanza Darasa la Elimu ya Awali akiwa na umri wa miaka mitano. Katika Elimu ya Awali mtoto atajifunza stadi za kuhusiana, kusoma, kuandika sanaa, ubunifu, michezo pamoja na stadi za awali za kuhesabu, sayansi na matumizi ya TEHAMA. Vilevile, mtoto atajifunza kuthamini utamaduni wa jamii yake, imani, tunu za taifa na utunzaji wa afya na mazingira.

Dira, Malengo na Umahiri wa Jumla

Mtaala huu umezingatia dira na malengo makuu ya elimu nchini Tanzania, malengo ya elimu ya awali na umahiri unaokusudiwa kujengwa kwa mtoto wa Darasa la Awali kama ilivyofafanuliwa katika vipengele vifuatavyo:

2.1 Dira

Kuwa na Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya, anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo katika kuleta maendeleo endelevu ya kitaifa na kimataifa.

2.2 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

- (a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;
- (b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;
- (c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;
- (d) Kuelewa na kulinda tunu za taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya taifa;
- (e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;
- (f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;
- (g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na
- (h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

2.3 Malengo ya Elimu ya Awali

Malengo ya Elimu ya Awali ni:

- (a) Kujenga misingi imara ya makuzi ya kimwili na uratibu wa misuli mikubwa na midogo;
- (b) Kukuza maadili na uwezo wa mtoto kuthamini na kudumisha tunu za taifa na utamaduni wa jamii yake;
- (c) Kukuza stadi za awali za lugha na mawasiliano (kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika), Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT), lugha mguso, na maandishi ya Breli;
- (d) Kukuza stadi za awali za ujifunzaji wa mtoto na tabia ya kupenda kujifunza;
- (e) Kujenga uwezo wa mtoto kijamii na kihisia;
- (f) Kukuza urazini na ujumi wa mtoto katika kutunza afya na mazingira;
- (g) Kukuza stadi za awali za kihisabati, kufikiri kimantiki, kutatua matatizo, ubunifu, uvumbuzi na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA);
- (h) Kubaini mtoto mwenye mahitaji maalumu na kutoa afua stahiki; na

- (i) Kumwezesha mtoto kuvuka salama kipindi cha mpito kutoka Darasa la Awali kwenda Darasa la Kwanza.

2.4 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Awali

Umahiri wa jumla umejikita katika ujenzi wa umahiri wa msingi katika kuwasiliana, kushirikiana, ubunifu, fikra tunduizi na utatuzi wa matatizo, ujuzi wa kidijiti na uzalendo ambao umefafanuliwa katika maeneo ya ujifunzaji kama ifuatavyo:

- (a) Utamaduni, Elimu ya Imani, Sanaa na Michezo;
- (b) Lugha na Mawasiliano;
- (c) Stadi za Awali za Maisha;
- (d) Afya na Mazingira; na
- (e) Stadi za Awali za Kihisabati, Sayansi na TEHAMA.

Maudhui ya Mtaala

Maeneo ya ujifunzaji na umahiri mkuu unaotarajiwa kujengwa katika Elimu ya Awali umebainishwa katika Jedwali Namba 1.1.

Jedwali Na.1. 1: Maeneo ya Ujifunzaji na Umahiri Mkuu

Na.	Maeneo ya Ujifunzaji	Umahiri Mkuu
1.	Utamaduni, Elimu ya Imani, Sanaa na Michezo	- Kumudu stadi za kisanii, ubunifu na Michezo - Kuthamini utamaduni wa jamii yake, elimu ya imani na tunu za taifa
2.	Lugha na Mawasiliano	Kumudu stadi za awali za lugha ya mawasiliano
3.	Stadi za Awali za Maisha	Kuhusiana
4.	Afya na Mazingira	Kutunza afya na mazingira
5.	Stadi za Awali za Kihisabati, Sayansi na TEHAMA	Kutumia stadi za awali za kihisabati, sayansi na TEHAMA

Maeneo ya ujifunzaji yamefafanuliwa kama ifuatavyo:

3.1 Utamaduni, elimu ya imani, sanaa na michezo

Eneo hili linajumuisha shughuli za kukuza na kuimarisha mwili ambazo hukuzwa kupitia shughuli za kisanii kama njia ya kuwasilisha ujumbe na ubunifu mbalimbali. Vilevile, eneo hili linamwezesha mtoto kutambua na kuthamini vitu vinavyohusiana na utamaduni wake kama vyakula, mavazi, sanaa za maonesho, na stadi za ubunifu zinazohusisha utendaji wa mwili ambao ni muhimu kwa afya njema. Mtaala huu unasisitiza watoto wajifunze imani zao ili kuwawezesha kujenga umahiri uliokusudiwa.

3.2 Lugha na mawasiliano

Eneo hili la ujifunzaji linamwezesha mtoto kujenga umahiri wa kuwasiliana katika miktadha mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Eneo hili pia humwezesha mtoto kuchangamana na wenzake, kusikiliza, kuzungumza na kupata stadi za awali za kusoma na kuandika.

3.3 Stadi za awali za maisha

Mtaala huu unalenga kukuza stadi za awali za maisha kwa mtoto ikiwa ni pamoja na kujitegemea, kujithamini na kuthamini wengine, kutawala hisia, kushirikiana na wengine, kuwasiliana, kufanya uamuzi sahihi na kutatua changamoto katika maisha ya kila siku. Hizi ni stadi muhimu zitakazomwezesha mtoto kumudu maisha ya kila siku.

3.4 Afya na mazingira

Eneo hili linamsaidia mtoto kuuelewa mwili wake na masuala mbalimbali yanayohusu afya. Baadhi ya masuala muhimu katika afya na maendeleo ya kimwili ni lishe bora, usafi binafsi na kanuni mbalimbali za afya. Vilevile, kwa upande wa mazingira, eneo hili litamsaidia mtoto kuthamini, kujali na kutunza mazingira yanayomzunguka. Aidha, litamwezesha mtoto kujenga uwezo wa kutambua maeneo hatarishi na kuchukua tahadhari kwa usalama wake na wa watu wengine.

3.5 Stadi za awali za kihisabati, sayansi na TEHAMA

Eneo hili linamwezesha mtoto kujiamini na kukuza ujasiri utakaomsaidia katika ngazi za elimu zinazofuata na maisha yake ya kila siku. Vilevile, litamsaidia kukuza stadi za kufikiri kimantiki, zitakazomsaidia mtoto kukuza uelewa wake na kumwezesha kufanya uamuzi sahihi. Stadi za msingi za kihisabati ni pamoja na kubaini maumbo, kulinganisha na kupima vitu, kuchambua na kupanga vitu kwa mfuatano unaolingana na kuhesabu. Stadi za msingi za sayansi ni kufanya majaribio sahili ya kisayansi, kuchunguza, kuwa na fikra tunduizi na kuvumbua. Aidha, eneo hili linamwezesha

mtoto kutumia vifaa vya TEHAMA kuwasiliana katika miktadha mbalimbali.
Umahiri mkuu na umahiri mahususi wa elimu ya awali umeainishwa katika Jedwali Na.1.2.

Jedwali Na.1. 2: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
1.0 Kumudu stadi za kisanii, ubunifu na michezo	1.1 Kuonesha sanaa za maonyesho 1.2 Kubuni sanaa zinazohusisha utendaji wa mikono 1.3 Kutumia stadi za ubunifu zinazohusisha utendaji wa mwili
2.0 Kuthamini utamaduni wa jamii yake, elimu ya imani na tunu za taifa	2.1 Kuthamini alama na tunu za taifa 2.2 Kuthamini vyakula vya Kitanzania 2.3 Kuthamini mavazi ya Kitanzania 2.4 Kuonesha matendo ya kiimani kulingana na imani yake 2.5 Kuheshimu imani za watu wengine
3.0 Kumudu stadi za awali za lugha ya mawasiliano	3.1 Kusikiliza katika miktadha mbalimbali 3.2 Kuzungumza katika miktadha mbalimbali 3.3 Kusoma katika hatua za awali 3.4 Kuandika katika hatua za awali 3.5 Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali
4.0 Kuhusiana	4.1 Kujithamini na kuthamini wengine 4.2 Kutawala hisia katika miktadha mbalimbali 4.3 Kumudu stadi za kujitegemea 4.4 Kumudu stadi za kushirikiana 4.5 Kutatua changamoto katika maisha ya kila siku
5.0 Kutunza afya na mazingira	5.1 Kutunza mwili 5.2 Kuthamini vyakula vya aina mbalimbali 5.3 Kutunza vyombo vya chakula 5.4 Kuchunguza vitu vilivyopo katika mazingira 5.5 Kusafisha mazingira 5.6 Kuepuka mazingira hatarishi 5.7 Kuchukua tahadhari dhidi ya magonjwa mbalimbali

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
6.0 Kutumia stadi za awali za kihisabati, sayansi na TEHAMA	6.1 Kutumia mazingira kujenga dhana za kihisabati na kufikiri kimantiki 6.2 Kufanya majaribio ya Kisayansi 6.3 Kutumia vifaa vya TEHAMA kuwasiliana katika miktadha mbalimbali

Ufundishaji, Ujifunzaji na Upimaji

Mtaala umebainisha jinsi ufundishaji na ujifunzaji utakavyofanyika, uchopekaji wa masuala mtambuka katika maeneo ya umahiri, muda anaotakiwa mtoto kujifunza na lugha ya kujifunzia na kufundishia, pamoja na upimaji wa maendeleo ya mtoto.

4.1 Ufundishaji na ujifunzaji

Mtaala huu unaelekeza matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazomfanya mtoto kuwa kitovu cha ujifunzaji na mwalimu kuwa mwezesaji. Mwalimu atatumia mbinu zinazomshirikisha mtoto katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai na uwezo wake. Mbinu zitakazotumika ni pamoja na matumizi ya michezo na sanaa, TEHAMA, majadiliano, matembezi darasani na mbinu zingine shirikishi zinazohamasisha ujifunzaji. Mtaala unasisitiza mwalimu kuwa mbunifu na mnyumbufu katika kutumia zana halisi zinazopatikana katika mazingira yake na kutengeneza mazingira ya mtoto kutumia zana hizo katika ujifunzaji.

4.2 Uchopekaji wa masuala mtambuka

Ufundishaji na ujifunzaji utahusisha uchopekaji wa masuala mtambuka kwa kuzingatia uhusiano kati ya suala mtambuka na umahiri unaotarajiwa kujengwa kwa mtoto kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 1.3.

Jedwali Na.1. 3: Masuala Mtambuka

Suala Mtambuka	Umahiri Mkuu					
	Kumudu stadi za kisani ubunifu na michezo	Kuthamini utamaduni wa jamii yake, elimu ya imani na tunu za taifa	Kumudu stadi za awali za lugha na mawasiliano	Kuhusiana	Kutunza afya na mazingira	Kutumia stadi za awali za kihisabati, sayansi na TEHAMA
Elimu Jumuishi	✓	✓	✓	✓	✓	✓

Suala Mtambuka	Umahiri Mkuu					
	Kumudu stadi za kisanii ubunifu na michezo	Kuthamini utamaduni wa jamii yake, elimu ya imani na tunu za taifa	Kumudu stadi za awali za lugha na mawasiliano	Kuhusiana	Kutunza afya na mazingira	Kutumia stadi za awali za kihisabati, sayansi na TEHAMA
Elimu ya Jinsia	✓	✓	✓	✓	✓	✓
Elimu ya Amani	✓	X	✓	✓	✓	X
Maadili	✓	✓	✓	✓	✓	✓
Haki na Wajibu wa Mtoto	✓	✓	✓	✓	✓	X
Haki za Binadamu	✓	X	✓	✓	✓	X
Ulinzi na Usalama	✓	✓	✓	✓	✓	✓
Usalama Barabarani	✓	X	✓	✓	✓	✓
Elimu ya Fedha	✓	X	X	✓	✓	✓
Elimu ya Rushwa	✓	X	✓	✓	✓	✓
Masuala ya Muungano	✓	✓	✓	✓	X	X

4.3 Muda wa kujifunza

Mwaka wa masomo una siku 194 sawa na wiki 39 zenye mihula miwili ya masomo. Muda wa ujifunzaji kwa siku ni saa tatu na nusu na muda wa kipindi ni dakika ishirini. Utaratibu wa siku, mgawanyo wa muda wa kujifunza na idadi ya vipindi kwa wiki vimefafanuliwa katika Jedwali Na. 1.4 na Na.1.5.

Jedwali Na.1. 4: *Utaratibu wa Ujifunzaji kwa Siku*

Shughuli za siku	Muda
Mduara wa asubuhi	Dakika 20
Shughuli za ujifunzaji	Dakika 80
Kona za ujifunzaji	Dakika 40
Kifunguakinywa	Dakika 30
Mapumziko	Dakika 30
Mduara wa kuagana	Dakika 10

Jedwali Na.1. 5: *Muda wa Ufundishaji na Ujifunzaji kwa Wiki*

Eneo la ujifunzaji	Umahiri Mkuu	Idadi ya vipindi kwa wiki	Muda wa kujifunza/ kutumia katika eneo la ujifunzaji (Dakika)
Utamaduni, Elimu ya Imani, Sanaa na Michezo	Kumudu stadi za kisanii, ubunifu na michezo	3	60
	Kuthamini utamaduni wa jamii yake, elimu ya imani na tunu za taifa	3	60
Lugha na Mawasiliano	Kumudu stadi za awali za lugha ya mawasiliano	5	100
Stadi za Awali za Maisha	Kuhusiana	2	40
Afya na Mazingira	Kutumia afya na mazingira	3	60
Stadi za Awali za Kihisabati, Sayansi na TEHAMA	Kutumia stadi za awali za kihisabati, sayansi na TEHAMA	4	80

4.4 Lugha ya kufundishia na kujifunzia

Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 Toleo la Mwaka 2023 inatamka kuwa lugha za Kiswahili na Kiingereza zitatumika kufundishia na kujifunzia katika elimu ya awali. Mtaala wa Elimu ya Awali umeandaliwa katika lugha mbili ambazo ni Kiswahili na Kiingereza. Aidha, Kiswahili kitatumika kama lugha ya kufundishia katika shule zinazotumia Kiswahili na Kiingereza kitatumika katika shule zinazotumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia.

4.5 Upimaji wa maendeleo ya mtoto

Mtaala huu unasisitiza upimaji unaozingatia vigezo vinavyotambulika vya upimaji wa maendeleo ya mtoto katika ukuaji na ujifunzaji wa kila siku. Upimaji unaotumika katika ngazi hii ni upimaji endelevu na hautahusisha mitihani ya kuandika wala kulinganisha watoto. Mtaala unajikita katika kupima maarifa, stadi na mwelekeo, ili kuhakikisha kwamba, upimaji unakuwa na ufanisi, mwalimu atamshirikisha mtoto mwenyewe, mzazi/mlezi na wadau wengine wa elimu katika upimaji. Aidha, mwalimu anatakiwa kufuatilia maendeleo ya mtoto katika nyanja zote kiakili, kimwili, kihisia na kijamii. Lengo la upimaji katika kipindi hiki ni kutambua maendeleo ya mtoto katika ukuaji na ujifunzaji pamoja na kubaini watoto wenye mahitaji maalumu na kutoa afua stahiki. Zana zinazotumika katika upimaji ni zile zitakazoweza kupima umahiri uliojengwa na mtoto ikiwemo uwezo wa kuwasiliana, kuhusiana, kutunza afya na mazingira na kutumia stadi za awali za kihisabati, kisanyansi na TEHAMA. Zana hizo ni pamoja na madodoso, orodhahakiki, fomu za kupima maendeleo ya mtoto na mkoba wa kazi.

Rasilimali za Utekelezaji wa Mtaala

Taratibu za utoaji wa Elimu ya Awali zitazingatia rasilimali, kanuni na miongozo inayotolewa na Wizara inayohusika. Upatikanaji wa rasilimali ni muhimu ili kutekeleza mtaala kwa ufanisi. Rasilimali hizo ni:

5.1 Rasilimali watu

(a) Mtoto

Mtoto ndiye mlengwa mkuu katika mtaala huu, hivyo utekelezaji wa mtaala utapaswa kuzingatia mahitaji, matakwa, umri na uwezo wa kila mtoto na utamaduni wake.

(b) Mwalimu

Mwalimu wa Elimu ya Awali anapaswa kuwa amepata mafunzo stahiki katika taasisi inayotambuliwa na serikali kwa sababu ndiye mtekelezaji mkuu wa mtaala huu. Katika kuleta ufanisi wa ufundishaji na ujifunzaji, Darasa la Awali linapaswa kuwa na mwalimu mmoja na msaidizi wa mwalimu mwenye sifa. Uwiano wa mwalimu kwa

watoto unapaswa kuwa 1:25. Mwalimu wa Elimu ya Awali anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

- (i) Aliyefuzu mafunzo ya ualimu wa Elimu ya Awali kuanzia ngazi ya Stashahada na kuendelea;
- (ii) Kuwa na maadili ya ualimu;
- (iii) Kuwa na ukarimu, upendo, uvumilivu na kujenga uhusiano mzuri na mtoto;
- (iv) Kuwajali na kuwapenda watoto wenye mahitaji maalumu;
- (v) Kuwa na urazini wa kutenda mambo kwa usahihi;
- (vi) Kujali muda na kuwa na mpangilio mzuri wa kazi za kila siku shuleni;
- (vii) Kunyumbuka na kuvaa uhusika wa mtoto wa Elimu ya Awali;
- (viii) Kujithamini na kuthamini wengine;
- (ix) Kuwa na stadi za karne ya 21;
- (x) Kushirikisha jamii katika kutoa huduma kwa watoto; na
- (xi) Awe na afya njema ya mwili na akili. Vilevile, anapaswa kuonesha cheti cha daktari.

Mwalimu wa Elimu ya Awali anapaswa kuwa na umahiri katika:

- (i) Kutafsiri na kutekeleza sheria, taratibu na miongozo iliyopo;
- (ii) Kutambua kipaji na kipawa cha mtoto na kukiendeleza;
- (iii) Kushirikisha wazazi/walezi katika kufanya utambuzi wa mapema na kutoa afua stahiki;
- (iv) Kutatua changamoto za ujifunzaji kwa mtoto;
- (v) Kuwawezesha watoto kujenga utayari wa kujifunza kwa vitendo;
- (vi) Kutumia stadi za TEHAMA katika kuwezesha ujifunzaji jumuishi;
- (vii) Kutumia stadi za unasihi na malezi katika kutatua changamoto za ujifunzaji;
- (viii) Kutambua mabadiliko ya tabia na hisia za watoto na kuwawezesha kujitawala;
- (ix) Kufanya tathmini binafsi;
- (x) Kupima maendeleo ya mtoto kwa kutumia zana stahiki;
- (xi) Kufanya tafakuri ya ujifunzaji wa mtoto na kutoa afua stahiki;
- (xii) Kufaragua na kutumia zana za kujifunzia;
- (xiii) Kutumia mrejesho kuboresha ufundishaji na ujifunzaji;
- (xiv) Kuandaa mazingira salama rafiki na wezeshi; na
- (xv) Kuandaa na kutumia mazingira ya ndani na nje kwa ufanisi.

(c) Msaidizi wa mwalimu

Darasa la Awali linapaswa kuwa na msaidizi wa mwalimu mwenye sifa stahiki atakayemsaidia mwalimu katika shughuli za kila siku. Aidha, msaidizi wa mwalimu anapaswa awe na afya njema ya mwili na akili. Majukumu ya msaidizi wa mwalimu ni pamoja na:

- (i) Kufanya maandalizi ya darasa ikiwemo kufanya usafi na kupanga vitu;
- (ii) Kufanya maandalizi ya kutengeneza na kufaragua zana za kujifunzia;
- (iii) Kutoa msaada kwa watoto wakati wa ujifunzaji ndani na nje ya darasa;
- (iv) Kutoa afua stahiki kwa watoto wenye mahitaji maalumu;
- (v) Kuandika na kutoa taarifa za maendeleo ya mtoto kwa mwalimu wa darasa; na
- (vi) Kuwatia moyo na kuwahimiza watoto kushiriki katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji.

5.2 Rasilimali vitu

Utekelezaji fanisi wa mtaala wa Elimu ya Awali unahitaji rasilimali vitu kama vile ardhi, samani na miundombinu pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Rasilimali hizo zinapaswa kuwa za kutosha na zinazokidhi viwango vya ubora vilivyobainishwa katika miongozo mbalimbali ya WyEST. Vilevile, zinapaswa kuzingatia mahitaji ya watoto wote wakiwemo wenye mahitaji maalumu.

(a) Ardhi

Ardhi kwa ajili ya uendeshaji wa Elimu ya Awali lazima iwe na hati miliki ya eneo, kibali cha ujenzi kutoka halmashauri, michoro na ramani ya shule iliyoidhinishwa na mhandisi wa majengo wa halmashauri, na taarifa ya tathmini ya mazingira kutoka kwa afisa mazingira wa halmashauri inayohusika.

Ukubwa wa ardhi unaotakiwa ili kuanzisha shule ya awali yenye madarasa yaliyojengwa kwa msambao ni nusu eka, na jengo la ghorofa ni theluthi ya eka. Mahitaji ya ukubwa wa eneo/ardhi kwa shule yenye mkondo mmoja litazingatia vipimo vya kiuhandisi vya majengo, viwanja vya michezo na eneo la wazi. Kuongezeka kwa eneo/ardhi la shule kutategemea ongezeko la mikondo.

(b) Samani na miundombinu

Utekelezaji wenye ufanisi wa Mtaala wa Elimu ya Awali unahitaji samani na miundombinu stahiki. Darasa la Awali linapaswa kuwa na samani za kutosha zilizotengenezwa kwa kuzingatia umri na mahitaji ya watoto wote wakiwamo wenye mahitaji maalumu. Samani hizo ni pamoja na mikeka, viti, na meza kulingana na umri

wa mtoto, pamoja na shubaka za kuhifadhi vitabu. Miundombinu inayopaswa kuwepo katika Elimu ya Awali ni pamoja na madarasa, maliwato, ofisi, uzio, jiko na maeneo kwa ajili ya michezo.

(c) Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia

Utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Awali unapaswa kuzingatia matumizi ya vifaa vya mtaala ambavyo vinaandaliwa na WyEST kupitia TET. Vifaa hivyo ni muhtasari, Mwongozo wa Mwalimu wa Kufundishia Elimu ya Awali na vitabu vya kiada, pamoja na vifaa vya TEHAMA. Aidha, mwalimu anapaswa kutumia vifaa/zana stahiki za kufundishia na kujifunzia zinazoendana na mahitaji ya mtoto. Ni muhimu zana zitengenezwe kutokana na rasilimali zinazopatikana katika mazingira yanayomzunguka mtoto.

5.3 Miongozo muhimu ya usimamizi na uendeshaji wa shule.

Utekelezaji wa Elimu ya Awali utafanikiwa kwa kutumia miongozo mbalimbali inayotambulika na serikali. Miongozo hii inasaidia kuwa na viwango sawa vya utoaji wa elimu nchini kwa kuzingatia taratibu, kanuni na sheria zilizopo. Ni muhimu kuwe na usimamizi imara kuanzia ngazi ya shule hadi wizara.

5.4 Rasilimali muda

Rasilimali muda ni muhimu katika utekelezaji wa mtaala. Muda wa utekelezaji wa mtaala huu umeelezewa katika kipengele cha 4.3 na Jedwali Na.1.5.

5.5 Rasilimali fedha

Upatikanaji wa rasilimali fedha ni muhimu katika uratibu, utekelezaji na uendeshaji wa Elimu ya Awali. Darasa la Awali kama yalivyo madarasa mengine lipatiwe ruzuku ili kuwezesha utekelezaji wa mtaala kwa ufanisi.

5.6 Ushiriki wa wadau katika utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Awali

Ushirikishwaji wa wazazi/walezi na wadau wa elimu ni muhimu sana katika kufanikisha ukuaji, ufundishaji na ujifunzaji wa mtoto wa Elimu ya Awali. Hawa ni wadau muhimu sana ambao wamekuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha utekelezaji wa mitaala nchini. Shule za awali hazina budi kushirikiana vyema na wadau hawa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa katika utoaji wa Elimu ya Awali.

SEHEMU YA PILI
MUHTASARI WA ELIMU YA AWALI

1.0 Utangulizi

Muhtasari wa Elimu ya Awali umeandaliwa kwa kuzingatia Mtaala wa Elimu ya Awali wa mwaka 2023. Muhtasari huu umezingatia nadharia za ukuaji na ujifunzaji, uwezo, umri na muktadha wa mtoto wa Kitanzania. Mwalimu anahimizwa kuwa mnyumbufu na mbunifu ili kumwezesha mtoto kujenga umahiri uliokusudiwa.

2.0 Maudhui ya ufundishaji na ujifunzaji

Muhtasari wa Elimu ya Awali umebeba maudhui ambayo yamepangiliwa katika vipengele sita ambavyo ni umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, vigezo vya upimaji, zana za kufundishia na kujifunzia na idadi ya vipindi. Jedwali lifuatalo linaonesha maudhui yanayopaswa kufundishwa katika ngazi ya Elimu ya awali.

Jedwali Na. 2.1: *Maudhui ya Muhtasari wa Elimu ya Awali*

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
1.0 Kumudu stadi za kisanii, ubunifu na michezo	1.1 Kuonesha sanaa za maonesho	(a) Kuimba nyimbo	Nyimbo zimeimbwa	Ala tofauti za muziki, nakala za nyimbo, vifani, vikaragosi, nyimbo zilizorekodiwa	30
		(b) Kughani mashairi	Mashairi yameghaniwa		
		(c) Kutamba ngonjera	Ngonjera zimetambwa		
		(d) Kuigiza	Maigizo yameigizwa		
		(e) Kutumia ala za muziki	Ala za muziki zimetumika		
		(f) Kucheza muziki	Muziki umechezwa		

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
	1.2 Kubuni sanaa zinazohusisha utendaji wa mikono	(a) Kuunda vitu	Vitu mbalimbali vimeundwa	Picha za video zinazoonesha namna ya kutengeneza vitu mbalimbali	46
		(b) Kuchora picha na maumbo	Picha na maumbo zimechorwa		
		(c) Kusuka vitu	Vitu mbalimbali vimesukwa		
		(d) Kutunga vitu katika uzi/kamba	Vitu vimetungwa katika uzi/kamba		
	1.3 Kutumia stadi za ubunifu zinazohusisha utendaji wa mwili	(a) Kucheza michezo inayohusisha misuli midogo	Michezo inayohusisha misuli midogo ya vidole imechezwa	Picha za mavazi ya michezo, drafti, bao, mchezo wa nyoka na ngazi, vibaofumbo, karata, mdako, ludo, kadi za kumbukumbu, bembea, ya kusukuma na mteleo, viunzi na tairi	39
		(b) Kucheza michezo inayohusisha misuli mikubwa	Michezo inayohusisha misuli mikubwa ya mwili imechezwa		
		(c) Kutengeneza vifaa vya michezo	Vifaa mbalimbali vya michezo vimetengenezwa		

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
2.0 Kuthamini utamaduni wa jamii yake, elimu ya imani na tunu za taifa	2.1 Kuthamini alama na tunu za taifa	(a) Kubaini alama za taifa	Alama za taifa zimebainishwa	Bendera ya taifa, picha ya twiga, vitabu vya picha zinazoonesha masuala ya muungano, chati ya picha inayoonesha viongozi wa kitaifa, fedha halisi za kitanzania, filamu zinazoonesha masuala ya muungano	28
		(b) Kubaini tunu za taifa (uzalendo, uwajibikaji na lugha ya taifa)	Tunu za taifa zimebainishwa		
		(c) Kuelezea Muungano wa Tanganyika na Zanzibar	Muungano wa Tanganyika na Zanzibar umeelezewa		
		(d) Kutaja majina ya viongozi wa kitaifa	Majina ya viongozi wa kitaifa yametajwa		
	2.2 Kuthamini vyakula vya Kitanzania	(a) Kubaini vyakula vinavyopatikana katika jamii yake	Vyakula vinavyopatikana katika jamii yake vimebainishwa	Picha/chati za vyakula mbalimbali, vyakula halisi Video zinazoonesha vyakula mbalimbali vya kitanzania	18
		(b) Kubaini vyakula vinavyopatikana katika jamii nyingine	Vyakula vinavyopatikana katika jamii nyingine vimebainishwa		

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
	2.3 Kuthamini mavazi ya Kitanzania	(a) Kubainisha mavazi ya Kitanzania yanayovaliwa katika mazingira yake	Mavazi ya Kitanzania yanayovaliwa katika mazingira yake yamebainishwa	Mavazi halisi, kadi zenye picha za mavazi, filamu zinazoonesha mavazi na vyakula mbalimbali	15
		(b) Kuonesha mavazi mbalimbali yanayovaliwa katika jamii yake	Mavazi mbalimbali yanayovaliwa katika jamii yake yameoneshwa		
	2.4 ¹ Kuonesha matendo ya kiimani kulingana na imani yake	(a) Kubaini imani yake	Imani yake imebainishwa	Mavazi ya aina mbalimbali kulingana na Imani, nguo halisi, picha za majengo ya kuabudia pamoja na picha zinazoonesha matukio ya kiimani	39
		(b) Kubaini matendo ya kiimani	Matendo ya kiimani yamebainishwa		

1 Umahiri mahususi huu utafundishwa na viongozi wa Imani husika katika kipindi cha dini

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
	2.5 Kuheshimu imani za watu wengine	(a) Kubainisha imani za watu wengine	Imani za watu wengine zimebainishwa	Picha za viongozi wa dini wakiwa katika mavazi yao, mavazi ya aina mbalimbali kulingana na imani, nguo halisi, picha za majengo ya kuabudia pamoja na picha zinazoonesha matukio ya kiimani	15
		(b) Kushirikishana katika shughuli za kijamii	Ameshirikiana katika shughuli za kijamii		
3.0 Kumudu stadi za awali za lugha na mawasiliano	3.1 Kusikiliza katika miktadha mbalimbali	(a) Kutofautisha sauti na milio katika mazingira yake	Sauti na milio katika mazingira yake imetofautishwa	Picha za vitu tofauti vinavyotoa mlio, vitabu vya hadithi, kadi za hadithi, vibao vya maelekezo, sauti mbalimbali za wanyama na ndege zilizorekodiwa vifani vya wanyama na vikaragosi	34
		(b) Kufuata maelekezo yanayotolewa	Maelekezo yaliyotolewa yamefuatwa		
		(c) Kusikiliza hadithi	Hadithi imesikilizwa		

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
	3.2 Kuzungumza katika miktadha mbalimbali	(a) Kusimulia matukio mbalimbali	Matukio mbalimbali yamesimuliwa	Picha za matukio tofauti, vitabu vya hadithi, picha za vitu mbalimbali, ala za muziki, nyimbo zilizorekodiwa	30
		(b) Kutega na kutegua vitendawili	Vitendawili vimetegwa na kuteguliwa		
		(c) Kuimba nyimbo	Nyimbo zimeimbwa		
		(d) Kusimulia hadithi	Hadithi imesimuliwa		
	3.3 Kusoma katika hatua za awali	(a) Kutumia stadi za awali za kusoma	Stadi za awali za kusoma zimetumika	Kadi za herufi, chati ya herufi, kadi za silabi, kadi za maneno kadi za picha, kadi za picha zenye maneno, vitabu vya picha, vibaofumbo vya herufi, sauti za herufi za irabu na konsonanti zilizorekodiwa	67
		(b) Kusoma picha	Picha zimesomwa		
		(c) Kutamka sauti za mwanzo za majina ya picha/maneno/vitu	Sauti za mwanzo za majina ya picha/maneno/vitu zimetamkwa kwa usahihi		

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
		(d) Kuhusianisha sauti na maumbo ya herufi	Sauti zimehusianishwa na maumbo ya herufi		
		(e) Kusoma silabi na maneno	Silabi na maneno yamesomwa		
	3.4 Kuandika katika hatua za awali	(a) Kufuatisha hatua za kuandika herufi	Hatua za kuandika herufi zimefuatishwa	Video inayoonesha namna ya kuandika herufi kwa kufuata hatua	35
		(b) Kuandika herufi	Herufi zimeandikwa	Chati inayoonesha hatua za uandishi wa herufi	
	3.5 Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali	(a) Kusalimiana na kuagana	Kitendo cha kusalimiana na kuagana kimefanyika	Picha zinazoonesha watu wakisalimiana na kuagana, picha zinazoonesha majengo mbalimbali kama vile: kanisa, msikiti, hospitali, shule, filamu zinazoonesha maeneo mbalimbali ya muhimu katika jamii	30

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
		(b) Kufuata kanuni za mawasiliano	Kanuni za mawasiliano zimefuatwa		
		(c) Kujieleza katika miktadha mbalimbali	Kujieleza kumefanyika katika miktadha mbalimbali		
4.0 Kuhusiana	4.1 Kujithamini na kuthamini wengine	(a) Kujitambulisha na kutambulisha wengine	Amejitalambulisha na kutambulisha wengine	Picha zinazoonesha watu wakijitambulisha na kutambulisha wengine, picha zinazoonesha matendo mema, picha zinazoonesha shughuli mbalimbali za kijamii, filamu zinazoonesha matendo mbalimbali ya kusalimiana kuagana na kutambulishana	18
		(b) Kuonesha matendo ya tabia njema	Matendo ya tabia njema yameoneshwa		
		(c) Kubaini haki na wajibu wake	Haki na wajibu umebainishwa		
		(d) Kubaini kazi zinazotendwa na wanafamilia na watu wengine	Kazi zinazotendwa na wanafamilia na watu wengine zimebainishwa		

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
	4.2 Kutawala hisia katika miktadha mbalimbali	(a) Kutaja vitu anavyovipenda na asivyovipenda	Vitu anavyovipenda na asivyovipenda vimetajwa	Picha zinazoonesha matendo ya hisia, picha za vitu mbalimbali, filamu zinazoonesha matendo ya hisia mbalimbali	16
		(b) Kueleza namna ya kutawala hisia	Namna ya kutawala hisia imeelezwa		
		(c) Kutenda matendo yanayoonesha hisia	Matendo yanayoonesha hisia yametendwa		
	4.3 Kumudu stadi za kujitegemea	(a) Kutenda matendo ya kujitegemea	Matendo ya kujitegemea yametendwa	Picha zinazoonesha matendo ya kujitegemea, picha zinazoonesha vitu katika mpangilio sahihi, vitu halisi, filamu zinazoonesha matendo ya kujitegemea	14
		(b) Kupanga vitu katika mpangilio sahihi	Vitu vimepangwa katika mpangilio sahihi		
	4.4 Kumudu stadi za kushirikiana	(a) Kushirikiana katika miktadha mbalimbali	Ameshirikiana katika miktadha mbalimbali	Picha zinazoonesha matukio ya kushirikiana, ludo, nyoka na ngazi, karata, drafti, vitabu vya hadithi kuhusu ushirikiano	13
(b) Kupeana zamu katika michezo na shughuli mbalimbali		Kupeana zamu katika michezo na shughuli mbalimbali kumefanyika			

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
	4.5 Kutatua changamoto katika maisha ya kila siku	(a) Kucheza michezo inayojenga stadi za kutatua changamoto	Michezo inayojenga stadi za kutatua changamoto imechezwa	Vibaofumbo, vipande vya mbao vya ukubwa tofauti	19
		(b) Kuonesha namna ya kukabiliana na changamoto	Namna ya kukabiliana na changamoto imeoneshwa		
		(c) Kutumia TEHAMA kutatua changamoto	TEHAMA imetumika kutatua changamoto		
5.0 Kutunza afya na mazingira	5.1 Kutunza mwili	(a) Kubainisha sehemu za mwili na kazi zake	Sehemu za mwili na kazi zake zimebainishwa	Picha/chati inayoonesha vifaa vya usafi wa mwili, chati inayoonesha sehemu za mwili, picha inayoonesha vifaa/sehemu za kuhifadhia nguo	22
		(b) Kusafisha mwili	Mwili umesafishwa		
		(c) Kutunza mavazi	Mavazi yametunzwa		

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
	5.2 Kuthamini vyakula vya aina mbalimbali	(a) Kubaini vyakula mbalimbali	Vyakula mbalimbali vimebainishwa	Picha za vyakula mbalimbali, vyakula halisi, picha zinazoonesha vifaa vya kuhifadhia chakula, vifani vya vyakula, picha zinazoonesha taratibu za kula katika miktadha mbalimbali	12
		(b) Kueleza taratibu za kuzingatia wakati wa kula	Taratibu za kuzingatia wakati wa kula zimeelezwa		
		(c) Kutunza vyakula	Vyakula vimetunzwa		
	5.3 Kutunza vyombo vya chakula	(a) Kutumia vyombo vya chakula	Vyombo vya chakula vimetumika	Picha za vyombo vya chakula, vifaa vya kuoshea vyombo vya chakula, picha zinazoonesha sehemu za kuhifadhia chakula	10
		(b) Kuosha vyombo vya chakula	Vyombo vya chakula vimeoshwa		
		(c) Kuhifadhi vyombo vya chakula	Vyombo vya chakula vimehifadhiwa		
	5.4 Kuchunguza vitu vilivyopo katika mazingira	(a) Kutaja vitu vinavyopatikana katika mazingira	Vitu vinavyopatikana katika mazingira vimetajwa	Picha/vifani vya vitu mbalimbali katika mazingira, picha za wanyama na mimea	24

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
		(b) Kutofautisha vitu katika mazingira yake	Vitu katika mazingira yake vimetofautishwa		
	5.5 Kusafisha mazingira	(a) Kufanya usafi katika mazingira yanayomzunguka	Usafi umefanyika katika mazingira yanayomzunguka	Picha zinazoonesha madhara ya mazingira machafu, vitabu vya hadithi vinavyoonesha madhara ya mazingira machafu	17
		(b) Kueleza madhara yanayotokana na mazingira machafu	Madhara yanayotokana na mazingira machafu yameelezwa		
	5.6 Kuepuka mazingira hatari	(a) Kubaini matendo hatari	Matendo hatari yamebainishwa	Picha zinazoonesha matendo hatari na mazingira hatari, picha inayoonesha alama za usalama	19
		(b) Kubaini mazingira hatari	Mazingira hatari yamebainishwa		
		(c) Kuonesha namna ya kuepuka mazingira hatari	Namna ya kuepuka mazingira hatari imeoneshwa		
		(d) Kubaini alama za usalama katika mazingira yake	Alama za usalama katika mazingira yake zimebainishwa		

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
	5.7 Kuchukua tahadhari dhidi ya magonjwa mbalimbali	(a) Kubaini magonjwa ya kuambukiza	Magonjwa ya kuambukiza yamebainishwa	Picha /chati zinazoonesha dalili za magonjwa ya kuambukiza, picha zinazoonesha namna ya kujikinga na magonjwa ya kuambukiza	15
		(b) Kujikinga na magonjwa	Amejikinga na magonjwa		
6 Kutumia stadi za awali za kihisabati, sayansi na TEHAMA	6.1 Kutumia mazingira kujenga dhana za kihisabati na kufikiri kimantiki	(a) Kubaini vitu vinavyojenga dhana ya namba katika mazingira	Vitu vinavyojenga dhana ya namba katika mazingira vimebainishwa	Kadi za namba, chati inayoonesha maumbo bapa, maumbo ya namba, chati za namba, sinia la namba, picha na fedha halisi za kitanzania	62
		(b) Kubaini maumbo	Maumbo yamebainishwa		
		(c) Kuchambua vitu kulingana na sifa	Vitu vimechambuliwa kulingana na sifa		
		(d) Kubaini vipimo	Vipimo vimebainishwa		
		(e) Kuhesabu namba 1-20	Namba 1-20 zimehesabiwa		
		(f) Kuandika namba 1-20	Namba 1-20 zimeandikwa		

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
		(g) Kuongeza kwa kutumia vitu halisi na TEHAMA	Kuongeza kwa kutumia vitu halisi na TEHAMA kumefanyika		
		(h) Kupunguza kwa kutumia vitu halisi na TEHAMA	Kupunguza kwa kutumia vitu halisi na TEHAMA kumefanyika		
		(i) Kutambua sarafu na noti za Kitanzania kuanzia sh 50 hadi sh 10000	Sarafu na noti za Kitanzania kuanzia sh 50 hadi sh 10000 zimetambuliwa		
	6.2 Kufanya majaribio ya Kisayansi	(a) Kuchunguza vitu katika mazingira yanayomzunguka	Vitu katika mazingira yanayomzunguka vimechunguzwa	Picha za mimea na wadudu Video inayoonesha majaribio sahili ya kisayansi	42
		(b) Kufanya majaribio sahili ya kisayansi	Majaribio sahili ya kisayansi yamefanyika		

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za ujifunzaji	Vigezo vya upimaji	Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	Idadi ya vipindi
	6.3 Kutumia vifaa vya TEHAMA kuwasiliana katika miktadha mbalimbali	(a) Kubaini vifaa vya TEHAMA	Vifaa vya TEHAMA vimebainishwa	Picha inayoonesha vifani mbalimbali vya TEHAMA	52
		(b) Kuunda vifani mbalimbali vya TEHAMA	Vifani mbalimbali vya TEHAMA vimeundwa		
		(c) Kutumia kompyuta kufanya shughuli mbalimbali	Kompyuta imetumika kufanya shughuli mbalimbali		
		(d) Kutumia vifaa mbalimbali vya TEHAMA	Vifaa mbalimbali vya TEHAMA vimetumika		

Bibliografia

- Ministry of Education and Culture. (2004). *National curriculum guidelines on early childhood education and care in Finland*. Finish National Agency for Education.
- Ministry of Education Culture and Human Resources. (2009). *National curriculum framework: Pre-primary 3-5 years*. Mauritius Institute of Education and Early Childhood Care and Education.
- National Board of Education in Finland (2000). *Core curriculum for pre-school education*. University Press Helsinki.
- Republic of Ghana (2018). *National pre-tertiary education curriculum framework for developing subject curricula*. Ministry of Education.
- Republic of Kenya (2019). *Basic education curriculum framework: nurturing every learner's potential*. Kenya Institute of Curriculum Development.
- Republic of Namibia. (2015). *Pre-primary syllabus english version*. Ministry of Education.
- Republic of South Africa. (2015). *The South African National Curriculum Framework for Children from Birth to Four*. Department of Basic Education.
- Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. (2022). *Muungano wa Tanganyika na Zanzibar: Chimbuko, Misingi na Maendeleo*: URT.
- Taasisi ya Elimu Tanzania. (2022). *Ripoti ya maoni ya wadau kuhusu uboreshaji wa mitaala ya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu*. Tanzania Institute of Education.
- Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (2016). *Mtaala na Muhtasari wa Elimu ya Awali*. Taasisi ya Elimu Tanzania.